Creating Knowledge. Inspiring Action.

Sisi ni kinanani?

FreshWater Watch ni shirika linaloendeshwa na taasisi ya Earthwatch (Ulaya). Taasisi ya Earthwatch (Ulaya) inaendesha shughuli za elimu ya uhifadhi na mambo ya utafiti, na limesajiliwa nchini England na Wales kwa namba 1094467, na kwa kampuni namba 4373313. Sisi ni wadhibiti wa takwimu na tumesajiliwa ofisi ya kamishna Z8787682.

Tunaamini kuwa tunaweza kuilinda dunia yetu ya asili kwa kufanya kazi pamoja. Tutafanya haya kwa mazingira yetu yakizingatiwa na sayansi. Tunatoa misaada kwa wanafunzi na wanasayansi waliochini kiuchumi, tunaelimisha kizazi kijacho na walimu wa shule, tunashirikisha wafanyabiashara na tunaijengea uwezo jamii kuchukua hatua pia.

Watu wanaotuunga mkono wanaamini kuwa kile tunachokifanya ni muhimu, na wanatusaidia kwa:

- Kuwa sehemu ya jumuiya ya Earthwatch na kujiunga na jumuiya ya jamii ya watu wanaochukua hatua Zaidi kwa dunia endelevu.
- Kutunisha mfuko na kuchangia pesa mbalimbali.

Jinsi tunavyotumia taarifa za wanaotuunga mkono

Ni jukumu letu kulinda na kuheshimu usiri wako na kutunza taarifa zako binafsi kwa kuzingatia kanuni na sheria za kutunza takwimu.

Hii ina maanisha kuwa:

Watoto

Kama una umri chini ya miaka 16, tafadhali hakikisha kuwa una ruhusa kutoka kwa mzazi au mlezi wako kabla ya kutupatia maelezo yako binafsi. Watoto walio chini ya miaka 16 hawaruhususiwi kutoa maelezo yao binafsi bila ruhusa hii.

Tunaweza kutumia taarifa zako biafsi kwa sababu mbalimbali:

Kuwa mwanachama wa FreshWater Watch:

Jina lako, eneo la kijiografia, na picha ya ukurasa wako vitaonekana kwenye ramani yetu ya takwimu wakati wa kukabidhi sampuli za ubora wa maji.

Tunashauri ubadilishe jina na kutumia jina ambalo utakuwa huru kulitumia kwenye mtandao. tunahitaji taarifa za eneo lako la kijiografia ili kuhakikisha tunaweka takwimu za FreshWater Watch ambazo ni sahihi kwa utafiti wetu. Takwimu zako za kisayansi ulizokusanya zitalinganishwa na kushirikishwa kwenye kurasa mbalimbali za kisayansi kama vile FreshWater Watch.

Kujiunga na Water Blitz. kama utajisajili kujiunnga na water Blitz tunahakikisha tunalinda na kutumia taarifa zako za posta kwa watu tunaowaamini ili kutusaidia kutuma vifaa vya Water Blitz. Maelezo Zaidi utayapata wakati wa kujisajili. Wadau hawa hawataweza kutumia taarifa au takwimu ulizokusanya kwa sababu za kibishiara.

Kutuma taarifa kuhusu FreshWater Watch na Earthwatch, wanufaika na wanaotuunga mkono, na shughuli ambazo utashiriki , mahali tunaporuhusiwa au vinginevyo. Unaweza kuchagua muda wowote.

Kuchakata michago ya kisayansi au uchagiaji uliofanya, kukushukuru na kukupa taarifa juu ya matokeo uliyofanya.

Kuandaa na kusimamia matukio

- Kusimamia mashindano ya kuingia.
- Kuuliza washiriki kuhusu shughuli na programu zetu kwa majibu ili kutusaidia katika soko letu la kitafiti na kuendeleza shughuli zetu.
- Kujibu maswali, malalamiko na ushauri.
- Kukuonyesha taarifa ambazo ni sahihi na za kweli kwa manufaa yako.
- Kuhifadhi muitikio kwenye kumbukumbu zetu.
- Kuhakikisha hatutumi taarifa ambazo hazihitajiki kwa watu wetu wanaotuunga mkono au wanachama wetu ambao wametuarifu kuwa hawatataka mawasiliano yoyote na sisi.
- Kutuma vifaa vya FreshWater Watch.

Mitandao ya kijamii.

Tunaweza kutumia anwani yako ya barua pepe ili kuilinganisha na ukurasa wako wa facebook au mitandao mingine ya kijamii ili kukuonyesha shughuli zako za Earthwatch wakati wa kutumia huduma hizi. Tutafanya hivi endapo tu tutachagua kutumia anwani yako ya baruapepe na tutatunza takwimu zako kwa usalama. Hakuna takwimu zako zozote ambazo zitasambaznwa kwa watu wengine.

Kuna njia mbili za kuzuia matumizi ya takwimu zako, unaweza kurekebisha chaguo lako kwenye Earthwatch kwa kuchagua channel za mawasiliano au unaweza kufanya hivi kwa kutumia mitandao ya kijamii.
Facebook: https://www.facebook.com/help/568137493302217
LinkedIn: https://www.linkedin.com/help/linkedin/answer/62931
Twitter: https://business.twitter.com/en/help/troubleshooting/how-twitter-ads-work.html

Kurekebisha uchaguzi wako kwenye Earthwatch hakumaanishi kuwa hautaona taarifa za Earthwatch kwenye mitandao ya kijamii, kwa sababu mitandao ya kijamii inaweza kurusha taarifa zako kulingana na vigezo vingine na si kwa sababu taarifa zako zimetolewa na Earthwatch.

Taarifa tunazoweza kukusanya kutoka kwako.

Wakati utakapojisajili kwenye mtandao tutakusanya taarifa ambazo zitahusiana na aina ya shughuli unazozifanya pamoja na maelezo Zaidi kama vile jina lako, anwani ya baruapepe, anwani ya posta na taarifa za benki kwa ajili ya kufanya malipo.

Wakati utakapofanikiwa kujiunga na programu au shughuli zetu, tunaweza kukuuliza kuhusu afya yako. Tunafanya hivi kuhakikisha kuwa tunasambaza vifaa na kutoa ushirikiano wa kutosha, na kuhakikisha kuwa wafanyakazi wetu wanajiandaa kujibu maswala kwa usahihi. Maelezo maalum yatatolewa wakati taarifa hizi zitakapotolewa. Taarifa zote binafsi zitatunzwa kwenye kumbukumbu maalum, ambazo watu maalum tu ndio wataweza kuzipata au Zitafutwa endapo hazitahitajika kutumika tena.

Endapo itatokea kutahitajika kutoa taarifa za mwanachama kwa manufaa yake mwenyewe, kwa mfano kupitia hospitali, tunaweza kufanya hivyo. Maelezo maalum ya sera hii yatapatikana kama utajiunga na programu yetu moja au shughuli zetu.

Kama utaweza kutuunga mkono Earthwatch katika mtindo endelevu, tunaweza kukupa mtaalamu wa akaunti ili kuendeleza uhusiano wetu. Kama hivi ndivyo tunaweza kukusanya taarifa zako binafsi kwa uhusiano wetu, kwa mfano mtizamo wako wa kisiasa au dini. Utatupa taarifa zote kuhusu afya yako na ya familia yako, hizi pia zinaweza kurekodiwa ili tuweze kuwasiliana nawe kwa wakati na njia inayofaa.

Tutaweka kumbukumbu ya picha, audio na video ambazo zinaweza kuwa taarifa binafsi chini ya sheria za umoja wa Ulaya. Tafadhali angalia vigezo na masharti ya sera yetu kwa maelezo ya leseni yetu kwa vitu vyote vinavyochangiwa kwenye tovuti yetu.

Sheria maalum ya kuchakata takwimu.

Ili kuendana na sheria ya utunzaji takwimu wa UK, Ni lazima kuwa na sababu maalum ya kukusanya na kutumia taarifa zako binafsi.

Msimamo wa kisheria ambao tutautumia unategemea na jinsi tutakavyokusanya na kutumia takwimu zako. Katika uchakataji wetu wa takwimu utakuwa katika vipengele vifuatavyo:

Utakapotupa ruhusa ya kutumia takwimu zako ulizokusanya kwa njia yoyote ile.

- kutuma taarifa kwetu kwa njia yoyote uliyoichagua.
- Kujibu maswali, malalamiko au mapendekezo mbalimbali.

Wakati wa kujaza taarifa zako binafsi ni muhimu kubeba mkataba huu wa kazi.

- Kushughulikia matukio na mafunzo mbalimbali.
- Kusimamia viingilio vya mashindano.

Wakati wa kutoa taarifa zako binafsi ni muhimu kwetu sisi kuendana na vigezo vya kisheria.

- Ni wajibu wetu kuhakikisha taarifa sahihi, hifadhi taarifa za kifedha kwa ukaguzi.
- Ni wajibu wetu kuhakikisha taarifa za mshiriki kwa usalama Zaidi.
- Ni wajibu wetu kuwajali washiriki wetu wa Earthwatch katika mafunzo na ujuzi mbalimbali n.k.

Wakati tutakapokuwa na nia ya kuwasiliana na wewe ili kukuza mfuko wetu kwa maendeleo ya kuhifadhi rasilimali za dunia. Mapendekezo yetu yanaweza kuwa kati ya yafuatayo:

- Kukutumia taarifa kuhusu Earthwatch, kwa ajili ya shughuli ulizoshiriki au kuuliza mrejesho wa shughuli ulizokuwa umeshiriki. Unaweza kuchagua muda na wakati wowote.
- Kukushukuru na kukujulisha matokeo ya ushiriki wako katika sayansi na michango uliyotoa.
- Kutunza taarifa katika mfumo wetu wa takwimu, kuhifadhi na kutunza taarifa za watu wetu wanaotupa taarifa na hawahitaji kuwasiliana nasi ili kuhakikisha hatutumi taarifa ambazo sio sahihi.

Kutumia taarifa za mtu binafsi.

Hatuuzi wala kutoa taarifa za mtu binafsi.

Tunaweza kuchangia baadhi ya taarifa kwa watu tunaowaamini ambao wanatusaidia kuchakata takwimu, kuandaa na kutuma mawasiliano au kuandaa taarifa za michango na nyinginezo.

Ni wajibu wetu kuhakikisha tunapata taarifa za hivi karibuni kuhusu watu wetu wanaotuunga mkono (mf.kama umehamia nyumba mpya, tunawajibu wa kuiondoa anwani yako ya zamani). Kuanzia sasa tutakuwa tunauliza watu tunaowaamini kwa ajili ya kusafisha takwimu zetu kwa ajili ya watu wanaotuunga mkono. Hii inamaanisha kuwa washiriki wetu wanaotupa takwimu watatumia taarifa ambazo zipo kwa uwazi kama vile anwani ya posta na anwani za watu ambazo wameondoa anwani zao za hivi karibuni.

Tuna wajibu wa kuwajali washiriki wetu kwa ujuzi, mafunzo mbalimbali n.k yanayoandaliwa na Earthwatch . Wakati wa dharura tunaweza kutumia taarifa binafsi na taarifa za kimatibabu ili kulinda manufaa yako binafsi.

Kusambaza taarifa binafsi.

Kama una mapendekezo yoyote kuhusu Earthwatch au kuuliza masuala yoyote kwa wakati ujao, unaweza kufanya hivi katika tovuti yetu inayomilikiwa na office yetu ya America Earthwatch.org (Earthwatch Institute (United States) 114 Western Avenue, Boston, MA 02134, U.S.A. Email: info@earthwatch.org). kumbukumbu ya taarifa zako binafsi zitatunzwa kwa sera hii.

Kwa vikundi vyote vinavyofanya kazi za sayansi shirikishi katika miradi ya kimataifa, hii inamaanisha kuwa mshiriki kutoka eneo Fulani anaweza kutia sahihi kwenye mradi (pamoja na kukabidhi taarifa binafsi, taarifa makini za kimatibabu kuhusu wao wenyewe) kupitia upande mmoja kwa mradi ambao unasimamiwa na mwingine. Kwahiyo ni muhimu kwa takwimu alizokusanya mshiriki kuchangiwa na vikundi kwa sababu za kiutawala na pia kumlinda mhusika wakati tukio lolote litakapotokea ambalo litahitaji kujua taarifa binafsi za mshiriki pamoja na taarifa za kimatibabu.

Endapo utafanikiwa kujiunga na programu au shughuli zetu, tunaweza kukuuliza taarifa za afya yako, mzio na mahitaji ya lishe kwa ujumla. Tutachangia taarifa hizi pamoja na wawezeshaji wetu kwa ajili ya makazi.

Tunavyo vigezo na mikataba tayari kwa kila mmoja ili kuhakikisha kuwa wanalinda na kutunza takwimu zako kwa usalama Zaidi.

Je tutatunza taarifa binafsi kwa muda gani.

Tutatunza taarifa zako binafsi kwa muda mrefu na kwa kadri tutakapozihitaji.

Watumiaji wa taarifa zetu.

Kwa washiriki wetu wa Earthwatch ambao watachagua kupokea mawasiliano yetu kama vile baruapepe, matangazo yetu, kwa kufanya kazi kwa kutumia huduma za baruapepe tutawaondoa watumiaji ambao hawafungui baruapepe zetu, au kutokujibu jumbe tunazowatumia kwa kipindi cha miaka miwili. Unaweza kuchagua kuwa utapokea barua-pepe zijazo kabla ya miaka miwili kuisha.

Wananchi Wanasayansi

Tunaamini katika kuchukua hatua za kisayansi ili kulinda dunia yetu ya asili. Kwa washiriki wetu wa Earthwatch ambao watashiriki katika mradi na kukusanya takwimu, tunaweza kuweka kumbukumbu za baadhi ya taarifa ambazo zinahusiana na utafiti wao wa kisayansi ili kuhakiki uhalali wa takwimu, majibu ya kisayansi na kwa tafiti zijazo. Katika hatua zote hizi ambapo hakuna umuhimu wa taarifa binafsi na taarifa za eneo kijiografia katika utafiti, tutaondoa maelezo ya sehemu hizo ingawaje tutahitaji kulipa eneo hilo utambulisho maalum ili kuweza kuziangalia takwimu kwa wakati ujao.

Washiriki wetu katika shughuli mbalimbali zinazofanywa na Earthwatch

Ni lazima tutatunza takwimu zako kwa miaka saba kwa ajili ya mahesabu na kujiridhisha.

Takwimu tulizokusanya.

Kama shirika lisilo na faida, Earthwatch inategemea michango ya fedha kutoka kwa wachangiaji na vikundi mbalimbali. Tunaweza kuchangia takwimu tulizokusanya kuhusu Earthwatch kwa jamii ili kuthibitisha matokeo yetu una kuwaonyesha wawezeshaji kwanini watuwezeshe kifedha. Hii haiambatani na taarifa binafsi za mtu yoyoyte ambazo zinaweza kumtambulisha kama mtu binafsi.

Tunaweza pia kuchakata takwimu zilizokusanywa kuhusu Erthwatch kwa jamii ili kutusaidia kuimarisha shughuli zetu za kiutendaji. Hii haiambatani na taarifa binafsi za mtu yoyoyte ambazo zinaweza kumtambulisha kama mtu binafsi.

Haki zako

Maombi ya taarifa.

Kama utapenda kuomba nakala ya taarifa zako ulizokusanya kwetu, tafadhali wasiliana na water@earthwatch.org.uk. Tafadhali tujulishe jina lako kamili na mradi ambao umeshiriki pamoja nasi. Tutashughulikia ombi lako ndani ya siku 30. Tunaweza kukuomba uthibitisho wa utambulisho wako.

Unahakikishiwa pia haki Zaidi chini ya sheria za ulindaji takwimu ambazo zimeainishwa hapa chini:

- Tutachakatata takwimu ulizokusanya endapo tu utakuwa umetoa ruhusa, una haki ya kukataa kutoa ruhusa muda wowote
- Una haki ya kubadilisha au kurekebisha taarifa zako binafsi endapo zitakuwa hazijakamilika au sio sahihi.
- Una haki ya kuomba taarifa zako binafsi zifutwe au ziondolewe katika mazingira fulani, mfano mahali ambazo zitakuwa hazina umuhimu tena kwetu kuzitunza au kwa sababu ya kuzichakata.
- Una haki ya kuzuia mchakato wa kuchakata takwimu zako kama kulikuwa hamna makubaliano ya usahihi au uthibitisho wa kuzitumia takwimu zako.
- Katika hatua Fulani, unaweza kuhamisha, kunakili na kusafirisha taarifa zako binafsi kirahisi na kiusalama kutoka mfumo wa mtandao mmoja kwenda mwingine.
- Una haki ya kuomba mchakato wa takwimu kulingana na manufaa yako kisheria.

Tafadhali zingatia kuwa haki hizi si lazima kutekelezwa kila wakati. Kwa mfano, taarifa binafsi hazitakiwi kufutwa kama zitakuwa zinahitajika kwa manufaa ya afya ya jamii au kutumika kisheria, kwa makualiano na kisayasi au kuweka historia za kitafiti.

Kwa maelezo Zaidi kuhusiana na haki hizi , tafadhali soma muongozo uliotolewa na ofisi ya kamishna wa habari.

Mabadiliko ya S**era.**

Sera hii inaweza kubadilika baada ya muda Fulani. Kwa mfano, tunaweza kurekebisha sera hii kulingana na mabadiliko ya sheria na kanuni.

Tafadhali tembelea tovuti kila mara ili kuweza kujua kama kua maadiliko yoyote yaliyotolewa kwenye matagazo yetu..

Kama kwa wakati wowote tutaamua kutumia taarifa zako iafsi kwa ajili ya utambulisho tofauti na jinsi tulivyozikusanya hapo awali, tutakujulisha kwa kutumia baruapepe. Watumiaji wanaweza kukubaliana kuchagua kutumia taarifa zao kwa njia hii ya tofauti.

Maelezo Zaidi

Tafadhali wasiliana nasi kwa maelezo zaidi au kama una maswali yoyote kuhusiana na sera hii. Tuandikie water@earthwatch.org.uk. Kama una maoni yoyote kuhusiana na Earthwatch inavyolinda na kutunza takwimu zake, tafadhali wasiliana nasi kwa privacy@earthwatch.org.uk au ofisi ya kamishna mkuu wa habari: 0303 123 1113.

Earthwatch Institute (Europe) is the working name for Conservation Education & Research Trust, a company limited by guarantee registered in England and Wales (no: 4373313) and a registered charity (no: 1094467).